TANGAZO LA SERIKALI NA. 191 limetolewa tarehe 15/3/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA. 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUNDA ("BUNDA WSSA"), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda ("Bunda WSSA"), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Machi 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Bunda WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 31 Mei 2019 au kabla, Bunda WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii.

(b) Bunda WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii.

(c) Bunda WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii.

(d) Bund WSSA itahakikisha kuwa taarifa zake za fedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) au mtu yeyote aliyeidhinishwa kutokana na kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kuhakikisha inawasilisha EWURA rasimu za mahesabu yaliyokaguliwa.

(e) Bunda WSSA itaweka mkakati wa kina wa kudhibiti upotevu wa maji na kuwasilisha andiko la mkakati huo kwa EWURA kabla ya tarehe 31 Juni 2019

(f) Bunda WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa.

(g) Bunda WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Bunda WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Bunda WSSA katika siku zijazo.

Kusitishwa kwa Amri

5. Amri hii linasitisha matumizi ya Amri Na. 11-014 la tarehe 1 Juni 2011 katika maeneo yanayohudumiwa na Bunda WSSA.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 800 | 1,500 | 1,860 | 1,900 |
| Taasisi | 1,200 | 2,190 | 2,660 | 2,690 |
| Biashara | 1,200 | 2,200 | 2,670 | 2,700 |
| Viwanda | - | 2,500 | 2,670 | 2,700 |
| Magati | 1,200 | 1,400 | 1,800 | 1,800 |
| Ujenzi | - | 2,700 | 2,700 | 2,700 |
| Kunywesha Mifugo | - | 2,600 | 2,600 | 2,600 |
| Wastani wa Bei | 950 | 1,683 | 2,075 | 2,109 |

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 1,000 | Wateja wa Bunda WSSA Hawatalipa Tozo ya Huduma | | |
| Taasisi | 1,000 | | | |
| Biashara | 1,000 | | | |
| Viwanda | 1,000 | | | |
| Magati | - | | | |
| Ujenzi | - | | | |
| Kunywesha Mifugo | - | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 32,000 | Asilimia ishirini (20%) ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2013 | | |
| Taasisi | 42,500 | | | |
| Biashara | 42,500 | | | |
| Viwanda | - | | | |
| Magati | - | | | |
| Ujenzi | - | | | |
| Kunywesha Mifugo | | | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 10,500 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Taasisi | 11,000 | 35,000 | 35,000 | 35,000 |
| Biashara | 11,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Viwanda | - | 35,000 | 35,000 | 35,000 |
| Magati | 11,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Ujenzi | - | 35,000 | 35,000 | 35,000 |
| Kunywesha Mifugo | - | 20,000 | 20,000 | 20,000 |

Jedwali Namba 1(e): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kupima Umadhubuti wa Dira (Shilingi/Upimaji)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | - | Ada ya Upimaji wa Dira Hairuhusiwi | | |
| Taasisi | - | | | |
| Biashara | - | | | |
| Viwanda | - | | | |
| Magati | - | | | |
| Ujenzi | - | | | |
| Kunywesha Mifugo | - | | | |

________

JEDWALI LA PILI

________

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | TZS Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| Ukarabati na Mabadilisho | | | | |
| Kununua pampu ya maji kwa ajili ya Kisima cha Kunzugu | | 25.00 | | 30 Juni 2020 |
| Kununua Dira za Maji 1,881kwa ajili ya mabadilisho | | 79.94 | 79.94 | 30 Juni 2020 |
| Kununua Mfumo wa Kompyuta wa Ankara | | 28.00 | | 30 Juni 2020 |

| | TZS Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| Kununua Samani za Ofisi (Viti na Meza) | 4.99 | 5.00 | 5.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua Kifaa cha Kutilia Klorini kwa ajili ya Kituo cha Kusukumua maji Migungani | 2.00 | | | 30 Juni 2019 |
| Jumla Ndogo (Ukarabati na Mabadilisho) | 6.99 | 137.94 | 84.94 | |
| Uwekezaji Mpya | | | | |
| Ujenzi wa Lango la Kudumu la kuchukulia maji Nyabehu | | 11.70 | | 30 Juni 2020 |
| Ujenzi wa Lango la Kuchukulia maji Guta Construction of Guta Intake | | 21.30 | | 30 Juni 2020 |
| Kutanua Mtandao wa Maji kwa Km. 24.3 hadi Ikizu Road, Bundastoo, Migungani, Bomani, Posta, Mwanza Road na Balili. | 91.25 | 50.00 | 298.00 | 30 Juni 2021 |
| Kujenga Mtandao wa Usambazaji wa Maji eneo la Tairo, Km.4 | | | 40.00 | 30 Juni 2021 |
| Kujenga Mtandao wa Usambazaji wa Maji eneo la Guta, Km.2 | 26.00 | | | 30 Juni 2020 |
| Kujenga Mtandao wa Usambazaji wa Maji eneo la Kilimahewa, Km.2 | | | 73.00 | 30 Juni 2021 |
| Kujenga Mtandao wa Usambazaji wa Maji eneo la Misisi, Km.3 | 30.00 | | | 30 Juni 2020 |
| Kujenga Mtandao wa Usambazaji wa Maji kutoka Nyasana hadi Viriani, Km.2 | | 178.18 | | 30 Juni 2020 |
| Kununua Vifaa vya Matengenezo kwa ajili ya kudhibiti Mivujo | 120.00 | 175.00 | 200.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua Dira Kuu za Maji | 9.00 | 3.00 | 3.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua Dira za Maji 6870 kwa ajili ya Wateja Wapya | | 258.57 | 325.38 | 30 Juni 2021 |
| Kununua Dira 1,146 za Malipo ya Kabla (Prepaid Meters) | | 201.60 | 402.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua Pikipiki 13 | 7.50 | 10.00 | 15.00 | 30 Juni 2021 |
| Jumla Ndogo (Uwekezaji Mpya) | 283.75 | 909.35 | 1,356.38 | |

| | TZS Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| Jumla ya Gharama za Uwekezaji | 290.74 | 1,047.29 | 1,441.32 | |

---

JEDWALI LA TATU

---

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

| Maelezo | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 1,600 | 3,000 | 3,800 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 40 | 35 | 30 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 87 | 90 | 95 |

________

JEDWALI LA NNE

________

MAHITAJI YA MAPATO YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI MILIONI)

| GHARAMA | Mahitaji ya fedha yaliyopendekezwa | | | Mahitaji ya fedha Yaliyoidhishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 202/21 | 2018/19 | 2019/20 | 202/21 |
| Uzalishaji wa Maji | 972.57 | 1,117.71 | 1,763.68 | 972.57 | 1,117.71 | 1,763.68 |
| Usambazaji wa Maji | 666.95 | 650.71 | 984.94 | 405.10 | 473.24 | 749.14 |
| Kuondoa Majitaka | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Matengenezo | 400.60 | 757.50 | 1,208.00 | 203.95 | 328.15 | 330.45 |
| Watumishi | 344.45 | 427.57 | 531.10 | 344.45 | 427.57 | 531.10 |
| Utawala | 254.63 | 346.37 | 435.53 | 226.13 | 309.80 | 379.72 |
| Matangazo | 9.54 | 10.02 | 10.52 | 9.54 | 10.02 | 10.52 |
| Matukio | 9.90 | 10.30 | 10.71 | 9.90 | 10.30 | 10.71 |
| Jumla (Uendeshaji na Matengenezo) | 2,659 | 3,320 | 4,944 | 2,172 | 2,677 | 3,775 |
| Ukarabati | - | - | - | 290.74 | 1,047.29 | 1,441.32 |
| Uwekezaji Mdogo | 0.30 | 53.14 | 89.65 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Jumla ya Gharama Zote | 2,659 | 3,373 | 5,034 | 2,462 | 3,724 | 5,217 |

Dodoma,
..................... 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Kaimu Mkurugenzi Mkuu*